

*Mulika, Na. 43 (1), 22-42
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ulinganisho wa Uingizaji wa Vidahizo Homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la Nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* Toleo la Kwanza

*Rehema Julius Magembe¹
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira
na
Perida Mgecha²
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira*

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.2>

Ikisiri

Makala haya yanalinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (KKS4) (2004) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza (KKF1) (2010). Malengo mahususi ya makala haya ni kueleza tofauti na ufanano unaojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu baina ya kamusi hizo mbili. Mbinu ya uchambuzi matini imetumika kupata data za makala haya. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Metaleksikografie ilioasisiwa na Weigand (1984). Matokeo yanaonesha kuwa kuna tofauti katika uingizaji wa vidahizo homonimu baina ya KKS4 na KKF1 ambazo zimejidhihirisha katika taarifa za kimatamshi, kietimolojia, uhusika wa vitenzi pamoja na uingizaji wa fasili za maana. Baadhi ya tofauti zinasababishwa na tofauti za kiutamaduni na maeneo ya kijiografia baina ya watumiaji wa kamusi teule ambamo lugha ya Kiswahili inatumika. Hata hivyo, makala haya yamedhihirisha kuwapo kwa ufanano wa uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1 katika vipengele vyta tahajia, matamshi, ubainishaji wa viambishi vyta umoja na wingi pamoja na ubainishaji wa viambishi vyta upatanisho wa kisarufi. Kwa ujumla, taarifa zilizoingizwa katika KKS4 ni nyingi kuliko taarifa zilizoingizwa katika KKF1. Hivyo, ni vyema kushughulikia katika matoleo yanayofuata ya kamusi hizi teule yale yanayoonekana kuwa ni tofauti zenye changamoto ili kuwa na kamusi zenye utoshelevu zaidi.

1.0 Utangulizi

Katika utunzi wa kamusi, suala la uingizaji wa vidahizo na usawidi wa taarifa zake za msingi huhitaji ujuzi wa kileksikografie. Makala haya yamejikita katika kulinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (KKS4) (2004) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza (KKF1) (2010). Matinde (2012) anaeleza kuwa kamusi ni kitabu chenye

¹ Baruapepe: magemberehema99@gmail.com

² Baruapepe: peridamgecha@gmail.com

mkusanyiko wa maneno sanifu katika lugha mahususi yaliyoorodheshwa kialfabeti na kutoa taarifa za kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata kisemantiki. Fasili hii inahusisha taarifa mbalimbali zinazowekwa katika kamusi, lakini yafaa kuzingatia kuwa si kamusi zote zina taarifa hizo. Kamusi ni kitabu chenye orodha ya msamiati ambao hukusanywa kutoka kwa wazungumzaji au matini mbalimbali na kuingizwa pamoja na taarifa zake kwa lengo la kukidhi mahitaji ya watumiaji husika. Aidha, homonimu ni maneno yenye maumbo sawa lakini maana na chanzo chake huwa tofauti (Kiango, 2017; Mlowezi na Mturo, 2019). Gichuri (2020) anasisitiza kuwa homonimu huwa hazina maana zenye uhusiano wa kihistoria wala chanzo kimoja. Hivyo, homonimu ni maneno yenye tahajia moja lakini huwa na maana tofauti zisizokuwa na uhusiano wa karibu.

Katika utunzi wa kamusi, zipo kanuni na taratibu zinazoelekeza namna gani taarifa za kileksikografia zinapaswa kuingizwa kulingana na malengo, aina ya kamusi na watumiaji wa kamusi husika (Mdee, 2010; Kiango, 2017). Pamoja na kuwapo kwa hiyo miongozo ya jumla, bado uingizaji wa vidahizo katika kamusi moja hutofautiana na wa kwenye kamusi nyingine hata kama zote ni za aina na lengo moja (Maithulia, 2021). Hivyo, makala haya yamelinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. Malengo mahususi ya utafiti huu ni: mosi, kueleza tofauti zinazojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu baina ya kamusi teule na pili ni kueleza ufanano unaojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu baina ya kamusi teule. Katika kutofautisha, vipengele vilivyohusishwa ni matamshi, etimolojia, uhusika wa kitenzi na fasili za maana. Katika ufanano, vipengele vilivyochunguzwa ni tahajia, matamshi, ubainishaji wa viambishi vya umoja na wingi pamoja na ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi.

2.0 Mapitio ya Maandiko

Tafiti mbalimbali zinazohusiana na uchunguzi wa kamusi zimefanyika. Miongoni mwa tafiti hizo ni ule wa Hans (2017) ambaye amechunguza changamoto zinazoweza kuwakabili watumiaji wa kamusi kwa mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). Hans amebaini changamoto zifuatazo: usanifu na urasmi wa maneno, athari ya lugha za kijamii katika Kiswahili, upatanisho wa kisarufi, dhana ya umoja na wingi na uingizaji wa majina ya maeneo. Makala haya yanatoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kukabiliana na changamoto hizi. Mapendekezo yaliyotolewa katika makala haya ni: mosi, kuwapo kwa baraza moja litakaloratibu matumizi sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa nchi zote za Afrika Mashariki. Pili, kuhusisha lahaja za Kiswahili na lugha za kijamii wakati wa usanifishaji wa maneno ya Kiswahili ili kupanua fasili za maana. Tatu, kuwa na kanuni zitakazoelewka wakati wa kuingiza taarifa mbalimbali katika kamusi, na nne, ni kuingiza maneno sanifu katika kamusi sanifu ilhali yale ambayo hayajasanifishwa yasubiri kwanza yasanifishwe ndipo yaweze kuingizwa katika kamusi. Maarifa ya makala haya yana mchango katika makala ya sasa kwani yamesaidia katika kuelewa

changamoto ambazo mtumiaji anazipata katika kutafuta maana za vidahizo ambapo homonimu ni sehemu ya vidahizo hivyo. Hans aliangalia changamoto zinazompata mtumiaji wa kamusi kwa ujumla kwa kurejea mifano kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) toleo la pili. Makala haya yanalinganisha kamusi mbili ambazo ni *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (2019) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) kwa kujikita katika kuangalia uingizaji wa vidahizo homonimu.

Vilevile, Maithulia (2021) amelinganisha namna kipengele cha urejeleano kilivyoshughulikiwa katika kamusi tatu za Kiswahili za lugha moja ambazo ni *Kiswahili Sanifu* toleo la tatu (2013), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016). Katika kipengele cha homonimu, utafiti huu umebaini kuwa katika kamusi teule zote tatu, kuna changamoto za uingizaji wa vidahizo homonimu ambapo kamusi moja imeingiza kama polisemi wakati huohuo kamusi nyingine imeingiza kidahizo hichohicho kama polisemia. Hali hii huweza kuwatatiza watumiaji hasa wale ambao lengo lao labda ni kufuatilia aina za vidahizo hivyo. Tofauti na utafiti wa Maithulia ambao umejikita katika kuchambua urejeleano katika utunzi wa kamusi, makala haya yamelinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1.

Aidha, Andrew (2016) ametafiti kuhusu uingizaji wa homonimu, polisemi na sinonimu katika *Kamusi la Kiswahili Fasaha* ya BAKIZA (2010). Utafiti wake umebainisha kuwa uingizaji na utumiaji wa homonimu, polisemi na sinonimu kwa kiwango kikubwa umezingatia nadharia za uingizaji na upangaji wa vitomeo katika kamusi. Anaendelea kufafanua kuwa homonimu katika kamusi hii zimeingizwa kwa kutumia namba za mfumo wa vimeo ili kuonesha kiwima idadi na utofauti mkubwa wa fahiwa zinazotokana na vidahizo vinavyohusika. Hata hivyo, Andrew anabainisha kuwa *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) imechanganya namna ya uingizaji wa baadhi ya vitomeo homonimu na polisemi. Kwa kusema hivyo anamaanisha kuwa baadhi ya homonimu zimeingizwa kama polisemi na baadhi ya polisemi zimeingizwa kama homonimu ilhali vidahizo hivyo havisawiri sifa husika. Licha ya utafiti wa Andrew kumakinikia uingizaji wa homonimu, polisemi na sinonimu katika kamusi moja, bado maarifa yanayohusu homonimu yamekuwa faafu katika kulinganisha uingizaji wa vidahizo hivyo katika KKS4 na KKF1.

Halikadhalika, Okal (2018) amefanya uhakiki linganishi wa taarifa muhimu kuhusu vidahizo katika *Kamusi ya Karne ya 21* toleo la kwanza na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la tatu. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa tahajia za kila kidahizo zimeoneshwa katika kamusi zote mbili. Kwa upande wa matamshi, Kamusi ya Karne ya 21 haikuungiza taarifa hiyo. Hii inatokana na kuwa uingizaji wa taarifa za vidahizo mara nyingi hutegemeana na malengo na walengwa wa kamusi husika. Pia, Okal aligusia aina za vidahizo kama homonimu, sinonimu na polisemi katika kipengele cha lugha kienzo iliyotumika kuingiza aina hizo za vidahizo; na kubainisha kuwa sinonimu zimeoneshwa kwa kutumia koma (,) na

homonimu zimeoneshwa kwa namba za kipeo. Kategoria za vidahizo vyote na wingi wa vidahizo nomino zimeoneshwa katika kamusi zote mbili huku kanuni na mbinu ya utoaji fasili za vidahizo zikizingatiwa vema. Kamusi zote zimeonesha matumizi ya vifupisho, tarakimu, alama mbalimbali, picha na michoro ili kurahisisha utoaji wa fasili za vidahizo. Utafiti huu una mchango katika makala haya katika kuelewa taarifa zinazoingizwa kwenye kamusi hasa za kisarufi na fasili za vidahizo ambazo zimesaidia katika kuchambua tofauti na ufanano wa uingizaji wa vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza.

Aidha, Kiango (2000) anabainisha njia mbalimbali za mpangilio wa maana katika kamusi ya lugha moja. Anafafanua kuwa maana za vidahizo zinaweza kupangiliwa kwa kufuata mpangilio ambao kwanza maana za msingi ndio hutangulia kisha maana zingine za ziada zinafuata. Pili, mpangilio wa maana kwa kuzingatia maana zisizokuwa za msingi zinawekwa baada ya maana za msingi. Tatu, mpangilio wa maana kwa utaratibu wa kimantiki. Nne, njia ya kupangilia maana kwa utaratibu wa majaribio; kwa maana ya kuanza na maana iliyozoleka kufuatiwa na maana ngumu ambazo hazifahamiki na wote. Tano, maana kupangwa kulingana na sifa za kisintaksia na sita ni njia ya kupanga maana katika mpangilio wa kihistoria. Mawazo haya yamewasaidia watafiti katika kuchambua tofauti za uingizaji wa maana za homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza.

Vilevile, Mdee (2010) anaeleza kuwa maana za vidahizo zinaweza kupangiliwa kwa namna tatu. Mosi, ni mpangilio wa kihistoria. Akimaanisha kwamba maana za awali za neno huorodheshwa kwanza na kufuatiwa na maana zilizotokea baadaye. Pili, ni mpangilio wa matumizi, yaani, maana ya neno ambayo hutumika mara kwa mara katika mawasiliano huorodheshwa kwanza na kufuatiwa na zile maana ambazo hutumiwa kwa uchache; yaani maana za awali za neno ambazo hazitumiki sana huorodheshwa mwisho katika orodha za maana. Maana za neno ambazo ni mahususi kwa fani fulani, huorodheshwa baada ya maana zenye matumizi mapana na tatu ni mpangilio wa maana msingi na maana ya ziada. Maana za neno huorodheshwa kwa kuzingatia maana ya msingi na maana za ziada zinazotokana na maana ya msingi. Andiko hili lina umuhimu kwani limeonesha namna fasili za maana za vidahizo zinavyopaswa kuingizwa na hivyo kuwaongeza maarifa watafiti katika kuchambua tofauti za uingizaji wa maana za vidahizo homonimu katika kamusi teule. Halikadhalika, Mdee anasisitiza kuwa maana ya kidahizo inapaswa kuelezwu kwa kutumia maneno ya kawaida yanayofahamika kwa wazungumzaji wengi wa lugha kisha yasiyofahamika. Anaendelea kueleza kuwa uepukaji wa maneno magumu katika fasili utamwezesha mtumiaji wa kamusi kuelewa maana ya kidahizo pale anapohitaji. Hivyo, kuna umuhimu wa kuingiza fasili za maneno ambazo hazitampa shida mtumiaji wa kamusi ili aweze kuelewa kwa ufasaha zaidi. Kutokana na hayo yote, makala haya yamelinganisha pia

kipengele cha uingizaji wa fasili za maana za vidahizo homonimu baina ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza.

Kama tulivyoona, zipo tafiti kadhaa zinazohusu uingizaji wa vidahizo katika kamusi na kuwapo kwa kanuni tangulizi zinazoongoza utunzi wa kamusi kama zilivyobainishwa na Kiango (2017) na Mdee (2010). Hata hivyo, bado kuna tofauti ambazo zinajitokeza katika uingizaji wa taarifa za msingi za vidahizo baina ya kamusi moja na nyingine hata kama zote zimejikita katika lengo kuu moja. Makala haya yamemakinikia kamusi mbili ambazo watanzi wake ni taasisi zinazojulikana kisheria. Hivyo, makala haya yamelinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (TUKI, 2019) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza (BAKIZA, 2010).

3.0 Nadharia Iliyotumika

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Metaleksikografija iliyoasisiwa na Weigand (1984). Nadharia hii inahusisha masuala yote ya kileksikografija. Nadharia ya Metaleksikografija imejengwa na misingi minne: wa kwanza ni historia ya leksikografija. Msingi wa pili ni uteuzi na matumizi ya kamusi, utoaji wa fasili za vidahizo na kanuni za utungaji wa kamusi, mpangilio wa vidahizo vya kamusi, na utafiti wa kileksikografija. Msingi wa tatu ni matumizi ya kamusi ambayo aghalabu huangazia sehemu ya utangulizi wa kamusi na tamati, na msingi wa nne ni uhakiki wa kamusi ambayo hurejelea vipengele anuwai vya lugha kienzo kama vile vya msimbo vinavyohusisha matumizi ya chapakoza ya kidahizo, kategoria ya kidahizo, othografia ya kidahizo, matamshi ya kidahizo, semantiki na matumizi ya kidahizo na kadhalika.

Makala haya yamezingatia zaidi msingi wa nne ambao unahuuhakiki wa kamusi. Msingi huu hurejelea vipengele anuwai vya lugha kienzo vinavyohusisha kuandika othografia ya kidahizo, matamshi ya kidahizo, kategoria ya kidahizo, semantiki ya kidahizo, matumizi ya kidahizo na kadhalika. Msingi wa tatu unaohusu matumizi ya kamusi pia umetumika. Msingi huu unasisitiza kuwa mwanaleksikografija anapaswa kufahamu kile ambacho mtumiaji wa kamusi anahitaji au taarifa ambayo mtu ye yeyote anaweza kuirejelea ili aweze kuiweka pale anapotoa fasili. Hivyo, nadharia hii imetumika katika kueleza tofauti na ufanano unaojitokeza katika uingizaji wa homonimu baina ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza. Utotofauti na ufanano huo umebainishwa kwa kuhakiki taarifa za kimatamshi, kietimolojia, uhusika wa kitende, fasili za maana, tahajia, ubainishaji wa viambishi vya umoja na wingi na ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi.

4.0 Methodolojia

Makala yanalinganisha uingizaji wa vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, toleo la kwanza.

Usanifu wa kifani umetumika katika makala haya. Usanifu huu umekuwa faafu katika kueleza kwa kina tofauti na ufanano unaojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu katika kamusi teule.

Sampuli ya makala haya ni kamusi mbili za Kiswahili: *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne ya TUKI (2019) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza ya BAKIZA (2010). Sampuli hizi ni faafu katika makala haya kwani kamusi hizo ndio matoleo ya mwisho kufanyiwa kazi. Kujikita katika sampuli hii, kumesaidia kutoa mchango wa mambo ya kufanyiwa marekebisho katika matoleo yanayofuata. Pia, kamusi hizi zimeteuliwa kwa kuwa ni kamusi zilizotungwa na vyombo rasmi vinavyotambuliwa kitaifa kuwa vina dhamana ya kutunga kamusi hizo.

Aidha, katika makala haya mbinu ya usampulishaji vigezo imetumika katika kuteua matini teule. Vigezo vilivyozingatiwa ni vinne. Mosi, ni kamusi ambazo ni matoleo ya mwisho kufanyiwa kazi ili kama kutakuwa na upungufu basi matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika kufanya marekebisho kwa matoleo yanayofuata. Pili, hizi ni kamusi zilizotungwa na taasisi zinazotambuliwa kisheria kwa kazi hiyo. Tatu, ni utofauti wa mazingira ya utunzi wa kamusi hizo, na nne, ni mapitio ya awali yenye viashiria vya kuwapo kwa vidahizo homonimu katika kamusi madhukura. Hivyo, usampulishaji vigezo umewasaidia watafiti kupata sampuli ya kamusi hizi mbili ambazo ni *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (2019) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza (2010) kwa ajili ya makala haya.

Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Data zilipatikana kwa kufuata hatua tatu. Kwanza, watafiti walisoma matini mwanzo hadi mwisho. Pili, walisoma tena na kuweka data katika makundi kulingana na malengo mahususi, na tatu, data zilichambuliwa kwa mbinu ya kusimbisha maudhui. Mbinu ya uchambuzi matini iliwezesha kupatikana kwa data za msingi kutoka kwenye matini teule. Vipengele vilivyotumika kuchambua matini hizi ni taarifa zilizoingizwa katika vidahizo homonimu. Katika kutofautisha, vipengele vilivyomakinikiwa ni: matamshi, etimolojia, uhusika wa kitensi na fasili za maana; katika ufanano, vipengele vilivyozunguza ni: tahajia, matamshi, ubainishaji wa viambishi vya umoja na wingi na ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi. Mbinu ya uchambuzi matini imefanikisha kupatikana kwa data zinazohusu tofauti na ufanano katika uingizaji wa vidahizo homonimu katika kamusi teule. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa mbinu ya kusimbisha maudhui. Katika mbinu hii, kwanza, data zilisomwa zaidi ya mara moja ili kubaini tofauti na ufanano wa uingizaji wa vidahizo homonimu baina ya kamusi teule. Pili, data ziligawanywa katika makundi mawili na kuwekewa misimbo (1 na 2), na tatu, misimbo inayolandana iliunganishwa ili kuunda sura ya kimaudhui kulingana na malengo mahususi. Data zinazoonesha tofauti ziliwekwa pamoja na zile zinazoonesha ufanano baina ya kamusi teule na ziliwasilishwa na kuchambuliwa kwa pamoja.

5.0 Matokeo na Mjadala

Sehemu hii inahusu tofauti na ufanano unaojitokeza katika uingizaji wa kidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne (2019) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza (2010). Kwanza, tumeanza kwa kueleza tofauti na ufanano wake. Uchambuzi umejikita katika kuangalia taarifa za kimatamshi, kietimolojia, uhusika wa kitenzi pamoja na fasili za maana za vidahizo homonimu.

5.1 Tofauti Zinazo jitokeza katika Uingizaji wa Kidahizo Homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la Nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* Toleo la Kwanza

Matokeo ya makala yamebaini kuwa baadhi ya homonimu zina tofauti katika uingizaji wa taarifa za kimatamshi, kietimolojia, uhusika wa kitenzi pamoja na fasili za maana. Katika makala haya, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne imetumia msimbo wa KKS4 wakati *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza imetumia msimbo wa KKF1.

5.1.1 Matamshi

Matamshi ni sauti zinazoingizwa kwenye kamusi ili kuwaelekeza walengwa wa kamusi namna kidahizo kinavyotamkwa (Kiango, 2017). Katika sehemu hii tumechambua data zinazoukilia tofauti za kimatamshi za kidahizo homonimu baina ya KKS4 na KKF1. Rejea data katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Tofauti za Kimatamshi katika Uingizaji wa Kidahizo Homonimu Bainya ya KKS4 na KKF1

Kidahizo Homonimu	Matamshi KKS4	Uk.	Matamshi KKF1	Uk.
chungu ¹	/'tʃungu/	85	/čungu/	58
chungu ²	/'tʃuŋgu/		/č ^h ungu/	
chungu ³	/'tʃuŋgu/		/č ^h ungu/	
dengua ¹	/dɛ 'ŋguwa/	95	/dɛ̄ nguwa/	65
dengua ²	/dɛ 'ŋguwa/		/dɛ̄̄ nguwa/	
dengua ³	/dɛ 'ŋguwa/		/d ^h ɛ̄̄ nguwa/	
gombea ¹	/gɔ'mbɛ̄ a/	151	/gombɛ̄ ja/	101
gombea ²	/gɔ'mbɛ̄ a/		/gombɛ̄ ja/	
hiari ¹	/hi'ari/	174	/hijari/	115
hiari ²	/hi'ari/		/hijari/	
jua ¹	/'juwa/	206	/juwa/	135
jua ²	/'juwa/		/juwa/	
koa ¹	/'kɔa/	296	/kowa/	190
koa ²	/'kɔa/		/k ^h owa/	
Nyambua ¹	/na'mbuwa/	495	/nambuwa/	309
nyambua ²	/na'mbuwa/		/nambuwa/	

Kidahizo Homonimu	Matamshi KKS4	Uk.	Matamshi KKF1	Uk.
yai ¹	/'jai/	733	/jaji/	461
yai ²	/'jai/		/jaji/	

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 1 lina data zinazoonesha tofauti zinazojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu kimatamshi katika KKS4 na KKF1. Ijapokuwa matamshi yanatofautiana, vidahizo vyote katika jedwali hilo vimejitokeza kama homonimu katika kamusi zote mbili. Kinacholeta utofauti katika uingizaji wa matamshi hayo ni uwasilishaji wa alfabeti *ch* ambapo katika KKS4 wametumia /tʃ/ wakati KKF1 imetumia /č/ na /čʰ/. Tofauti hii inatokana na sababu za kilahaja ambapo KKS4 imetumia matamshi ya Kiswahili kinachotumika Tanzania Bara ilhali KKF1 imetumia zaidi matamshi ya Kiswahili kinachozungumzwa Tanzania Visiwani. Pia, katika kuwakilisha ng, KKS4 wametumia sauti /ŋ/ wakati kwenye KKF1 wametumia /ng/. Vilevile, kuna uchopekaji wa viyeyusho /w/ na /j/ katika matamshi yaliyoingizwa kwenye KKF1 wakati kwenye KKS4 hakuna. Uchopekaji wa /w/ umejitokeza katika homonimu **koa¹**, **koa²** ambapo katika KKS4 matamshi yake yanafanana ambayo ni /kɔa/ lakini katika KKF1 matamshi ya **koa¹** ni /kɔwa/ na **koa²** ni /kʰɔwa/.

Homonimu **gombea¹** katika KKS4 ina matamshi /gɔ'mbɛ a/ wakati kwenye KKF1 ni /gombɛ ja/ tofauti ipo katika uchopekaji wa kiyeyusho /j/. Uchopekaji huu umefanya homonimu **hiari²** iingie katika kundi hili pia ambapo katika KKS4 ni /hi'ari/ na katika KKF1 ni /hijari/. Vilevile, homonimu **yai¹** imeingizwa kama /'jai/ katika KKS4 wakati kwenye KKF1 imeingizwa kama /jaji/. Katika uingizaji wa matamshi ya homonimu **gombea¹**, **hiari²**, **yai¹** katika KKF1 kuna uchopekaji wa kiyeyusho /j/ ambapo uwasilishaji huu unafanya matamshi yatofautiane katika kamusi moja na nyingine. Vilevile, data inaonesha kuwa sifa ya mpumuo imejitokeza katika homonimu za KKF1, mfano kidahizo **chungu²** kimeingizwa kama /čʰungu/ katika KKF1 na **koa²** kimeingizwa kama /kʰowa/. Data imedhihirisha kuwa sifa ya mpumuo inajitokeza mwanzoni mwa neno ilhali katika KKS4 sifa ya mpumuo haijajitokeza kabisa. Aidha, katika Jedwali Na. 1 data zinaonesha kuwa alama ya mkazo imejitokeza kwenye matamshi ya vidahizo vyote katika KKS4 wakati taarifa hii haijaingizwa katika KKF1.

Hivyo, kuna tofauti zinazojitokeza katika uingizaji wa taarifa ya matamshi kwa baadhi ya vidahizo homonimu vya KKS4 na KKF1 ambapo matamshi ya homonimu katika KKS4 yameingizwa kawaida wakati katika KKF1 kuna uchopekaji wa viyeyusho pale kidahizo kinapokuwa kimeundwa na mfuatano wa irabu mbili. MBAABU (2007) anapendekeza kuwa maneno ambayo herufi y iliwekwa katikati ya irabu mbili kwa sababu ya mvutano wa /e/ na /i/ yaandikwe bila y na w kati ya o na u na irabu nyingine idondoshwe. Kutokana na pendekzo hilo, kuna

uwezekano mkubwa wa kuepuka tofauti zinazojitokeza katika uchopekaji wa viyeyusho katika matamshi kwa kuzingatia mapendekezo hayo ya MBAABU. Aidha, katika KKF1 sifa ya mpumuo imejitokeza mwanzoni mwa vidahizo vnavyoanza na vipasuo kwa baadhi ya vidahizo homonimu wakati katika KKS4 taarifa hiyo haipo. Kuwapo kwa sifa ya mpumuo katika KKF1 na kutokuwapo katika KKS4, kunashadidiwa na Gichuru (2020) anaposema kuwa mpumuo hutumiwa kwa wingi na wazaliwa na wenyeji wa Pwani hasa katika lajaja za kaskazini kuliko za kusini kama Kiunguja. Anaendelea kusema kuwa labda ndiyo maana Kiswahili sanifu kimepuza mpumuo kwani kilisanifishwa kwa misingi ya Kiunguja. Hivyo, ni dhahiri kuwa fonolojia inabadilika na kupoteza sifa ya mpumuo polepole.

Halikadhalika, katika KKS4 mkazo umewekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho katika kila matamshi ya kidahizo homonimu lakini KKF1 haikuweka taarifa ya mkazo katika homonimu zote. Gichuru (2020) anasisitiza kuwa kila lugha huwa na mfumo wake wa mkazo. Kwa kawaida, lugha ya Kiswahili huweka mkazo katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno husika. Taarifa hii ni ya msingi katika kamusi zinazohusu lugha ambazo zina mkazo bainifu kama vile Kiswahili. Hivyo, ni vyema taarifa hii ikazingatiwa katika toleo lijalo la KKF kwani humsaidia msomaji au mtumiaji wa kamusi kutamka maneno kwa usahihi na ufasaha.

5.1.2 Etimolojia

Etimolojia ni taaluma inayohusu historia ya maneno na maana zake; huonesha historia ya neno tangu lilipoingia katika lugha hadi wakati linapoingizwa kwenye kamusi (Kiango, 2017). Katika makala haya, imebainika kuwa kuna tofauti za uingizaji wa taarifa za kietimolojia za vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. Katika makala haya, msimbo (-) umetumika kumaanisha kuwa taarifa hiyo haijaingizwa kwenye vidahizo homonimu vya kamusi husika. Rejea Jedwali Na. 2.

Jedwali Na 2: Tofauti za Kietimolojia katika Uingizaji wa Vidahizo Homonimu baina ya KKS4 na KKF1

Kidahizo	Etimolojia katika KKS4	Uk.	Etimolojia katika KKF1	Uk.
adhuhuri ¹ adhuhuri ²	(Kar) (Kar)	4	-	2
baa ¹ baa ² baa ³	(Kar) (Kng) -	28	-	14
chaki ¹ chaki ²	(Kng) -	65	-	41
desturi ¹ desturi ²	(Kaj) (Kaj)	96	-	65
enzi ¹ enzi ²	(Kar) (Kar)	113	-	78

Kidahizo	Etimolojia KKS4	katika	Uk.	Etimolojia KKF1	katika	Uk.
hodhi ¹	(Kar)		178	-		118
hodhi ²	-					
Kabuli ¹	(Kar)		211	-		138
kabuli ²	(Kar)					
ripoti ¹	(Kng)		550	-		347
ripoti ²	(Kng)					
tari ¹	(Kaj)		621	-		389
tari ²	(Kaj)					

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 2 hapo juu linaonesha kuwa kuna tofauti zinazojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1 kwenye kipengele cha etimolojia. Vidahizo hivyo vimetoka kama homonimu katika kamusi zote mbili hata kama KKF1 haioneshi etimolojia zake. Vidahizo **adhuhuri**, **enzi** na **kabuli** pamoja na homonimu zake vimeingizwa katika KKS4 vikiwa na taarifa ya kietimolojia ambayo ni (Kar) Kiarabu; wakati vidahizo homonimu **baa²**, **chaki¹** na **ripoti** pamoja na homonimu zake vina etimolojia ya (Kng) Kiingereza. Vilevile, **desturi** na **tari** ni vidahizo homonimu ambavyo vimeingizwa katika KKS4 vikiwa na etimolojia ya (Kaj) Kiajemi.

Kwa upande wa KKF1, tunaona taarifa za kietimolojia hazijaingizwa kabisa katika vidahizo vyote. Hii inawezekana halikuwa lengo la kamusi hii kuzingatia kipengele hiki hata kama taarifa hii ni ya muhimu katika vidahizo vile ambavyo vimepokea mabadiliko kadhaa kama vile ya kimatamshi, kiumbo, kimaana na kimatumizi au kwa vidahizo ambavyo vimetoka katika lugha nyingine nje na lugha ya kamusi husika. Hata hivyo, katika KKS4 kuna baadhi ya vidahizo homonimu ambavyo havijaingiziwa etimolojia (kama vile **liwa**, **tone** na **ongoa**). Pia, kuna vidahizo homonimu ambavyo etimolojia yake inatofautiana licha ya kuwa vinafanana kitahajia na kimatamshi, kwa mfano, katika Jedwali Na. 2 homonimu **baa¹** asili yake ni Kiarabu, **baa²** ni Kiingereza wakati **baa³** haijaingiziwa etimolojia yake. Tofauti ya uingizaji wa etimolojia katika KKS4, kwa vidahizo homonimu vilivyowekewa etimolojia inawezekana kuwa vidahizo hivyo asili yake imeshathibitishwa na tafiti mbalimbali wakati kwa vidahizo ambavyo havijawekewa inawezekana bado taarifa zake hazijathibitishwa kisayansi kama anavyosisitiza Kiango (2017). Hata hivyo, kutokuwekwa kwa taarifa ya etimolojia kwa baadhi ya homonimu inawezekana vidahizo hivyo haviwezi kuwatatiza watumiaji wa kamusi husika kutokana na asili au historia yake kuwa wazi kwa watumiaji. Katika makala haya imebainika kuwa vidahizo homonimu vingi vilivyowekewa etimolojia katika KKS4 ni vile vilivyokopwa au kutoholewa kutoka lugha nyingine nje ya Kiswahili.

Etimolojia ni taarifa ambayo huhitajika kuingizwa katika kamusi japo haizingatiwi sana na wasomaji walio wengi wa kamusi lakini ina umuhimu mkubwa kwa watafiti kama vile wanaofanya utafiti katika isimu historia. Pamoja na hayo, Nadharia ya Metaleksikografia inasisitiza kuzingatia etimolojia ya vidahizo kama taarifa ya msingi katika uundaji wa kamusi toshelevu. Kwa kuwa kuna uwezekano wa kuwa na msamiati ambao asili yake ni lugha nyingine, Okal (2018) anasisitiza kuwa katika kamusi ya lugha ya Kiswahili, kuna maneno ambayo yamechukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye lahaja, Kibantu na lugha nyingine za kigeni kama vile Kiajemi (Kaj), Kiarabu (Kar), Kihindi (Khi), Kijerumani (Kje), Kiingereza (Kng), Kireno (Kre) na kadhalika. Hivyo, taarifa hii ni muhimu kuwapo katika kamusi zote zinazohusu lugha ya Kiswahili kwani baadhi ya watumiaji huingia kwenye kamusi kwa ajili ya kuangalia asili ya neno tu.

5.1.3 Uhusika wa Kitenzi

Uhusika wa kitenzi ni hali ya kitenzi kutokana na maana pamoja na umbile lake kuhitaji au kutohitaji kukamilishwa na nomino (Haji, 2018). Uhusika wa kitenzi umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni vitenzi elekezi na vitenzi ambavyo sielekezi. Kitenzi ambacho kimatumizi ni lazima kifuatiwe na nomino kimepewa taarifa kuwa ni elekezi [ele] na kile ambacho kimatumizi hakihitaji kifuatiwa na nomino kimepewa taarifa kuwa sielekezi [sie]. Katika Jedwali Na. 3, msimbo (-) unamaanisha kuwa taarifa ya uhusika wa kitenzi haipo katika vidahizo homonimu vya hiyo kamusi.

Jedwali Na. 3: Tofauti za Uhusika wa Kitenzi katika Uingizaji wa Kidahizo Homonimu baina ya KKS4 na KKF1

Kidahizo Homonimu	Uhusika wa Kitenzi katika KKS4	Uk.	Uhusika wa Kitenzi katika KKF1	Uk.
angu.a ¹ angu.a ²	[ele] [ele]	20	-	10
bashiri ¹ bashiri ²	[ele] [ele]	38	-	22
chinj.a ¹ chinj.a ²	[ele] [ele]	78	-	51
fok.a ¹ fok.a ²	[sie] [ele]	127	-	86
isha ¹ Isha ² ish.a ³	- - [ele, sie]	189	-	125

Kidahizo Homonimu	Uhusika wa Kitenzi katika KKS4	Uk.	Uhusika wa Kitenzi katika KKF1	Uk.
pa.a ¹	[ele]	509	-	318
pa.a ²	[sie]			
pa.a ³	[ele]			
pa.a ⁴	[sie]			
paa ⁵	-			
paa ⁶	-			

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 3 lina data za uhusika wa kitenzi, zinazoonesha tofauti zinazojitokeza katika uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. Ijapokuwa vidahizo hivyo vyote vimejitokeza kama homonimu katika kamusi zote, taarifa ya uhusika imeingizwa katika KKS4 tu. Baadhi ya vitenzi homonimu vyenye sifa ya kuwa elekezi, vimewekewa alama ya [ele], vitenzi sielekezi vimewekewa alama ya [sie] wakati vile vyenye sifa zote mbili vimewekewa alama ya [ele, sie]. Alama hii (-) katika Jedwali Na. 3, imetumika kuonesha vidahizo homonimu ambavyo si kategoria ya vitenzi. Hii ni kwa sababu sifa ya uelekezi hurejelea vitenzi. Kwa upande wa KKF1, taarifa ya uhusika wa kitenzi haijaingizwa.

Pamoja na kuwa taarifa ya uhusika wa kitenzi haikutiliwa maanani katika KKF1, bado Nadharia ya Metaleksikografia inasisitiza kuwa taarifa hii ni mojawapo ya taarifa za msingi katika kamusi. Okal (2018) pia anasisitiza kuwa licha ya kuwapo kwa aina nyingi za vitenzi katika lugha, katika utungaji wa kamusi vitenzi huangaziwa kiuelekezi. Mdee na wenzake (2011) wanashadadia kuwa katika kamusi iwapo kitenzi kinaweza kufuatiwa na nomino kimatumizi basi ni kitenzi elekezi na iwapo hakifuatiwi na nomino au hakihitaji nomino moja kwa moja basi hurejelewa kama kitenzi si elekezi. Matokeo ya makala haya yanaonesha kuwa uhusika wa kitenzi ni taarifa ambayo imeingizwa katika KKS4 wakati katika KKF1 haijaingizwa kabisa. Hali hii pia imejitokeza katika vidahizo vingine ambavyo siyo homonimu. Suala la uhusika wa kitenzi ni la muhimu kwani huwasaidia watumiaji wa kamusi kuelewa kitenzi cha Kiswahili kwani ni kategoria mojawapo ambayo ni ya msingi inayodokeza kuwapo au kutokuwapo kwa mtendwa wa jambo katika kutumia lugha.

5.1.4 Fasili za Vidahizo Homonimu

Fasili ya kidahizo katika kamusi hurejelea maana ya kileksimu (Mdee, 2010). Kwa kutumia taarifa inayohusu kipengele cha fasili, tumechambua data na kueleza utofauti wa uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. Rejea data katika Jedwali Na. 4 zinazoonesha kuwapo kwa utofauti huo.

Jedwali Na 4: Tofauti katika Uingizaji wa Fasili za Vidahizo Homonimu Bainya ya KKS4 na KKF1

Kidahizo na Fasili yake katika KKS4	Kidahizo na Fasili yake katika KKF1
ghulamu¹ kijana mwanamume. (KKS uk. 147).	ghulamu¹ mtoto wa kiume anayefikia hadi umri wa miaka kumi na nane. (KKF uk. 98).
ghulamu² mzungu wa tatu katika mchezo wa karata. (KKS4 uk. 147).	ghulamu² karata yenye alama ya J au Q juu pembedi, upande wa kushoto na chini pembedi upande wa kulia ambayo ina thamani ya alama tatu kwa J au mbili kwa Q katika mchezo wa karata. (KKF1 uk. 98).
nyanya¹ aina ya tunda ambalo likiiva huwa jekundu na hutumika kwa kuungia mboga au kuliwa bila kupikwa.	nyanya¹ tunda dogo lenye umbo refurefu la rangi ya kijani nyepesi linalolimwa kuwa ni mboga. (KKF1 uk. 310).
nyanya² mama mzaa baba au mama. (KKS4 uk. 496).	nyanya² taz. bibi¹ (KKF1 uk. 310).
daka¹ nyaka kwa mikono kitu kilichorushwa au kitokacho juu kuja chini. daka² nafasi iliyofanywa ndani ya ukuta ili kuwekea kitu. daka³ - tunda ambalo halijakomaa k.v. nazi (KKS4 uk. 89).	daka¹ tunda la mnazi kabla halijawa na maji ndani. daka² = shubaku . daka³ kitendo cha kushika au kupokea kilichorushwa au kinachoanguka kutoka juu = nyaka (KKF1 uk. 60).

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Data za Jedwali Na. 4 zinaonesha kuwa homonimu **ghulamu¹** imeingizwa katika KKS4 ikiwa na maana fupi ambayo msomaji hawezu kuelewa kwa upana kinachozungumziwa wakati katika KKF1 imeingizwa ikiwa na maana ambayo ni toshelevu. Vilevile, **ghulamu²** imeingizwa katika KKS4 ikiwa na maana ambayo si toshelevu kwani haiko wazi kwa kuwa ndani yake imehusisha istilahi zinazohitaji kufafanuliwa tena (kama vile mzungu wa tatu) wakati katika KKF1 maana ilioingizwa ni ndefu na ya mzunguko na inamchanganya msomaji katika kuelewa maana halisi ya homonimu hiyo. Aidha, homonimu **nyanya¹** imeingizwa katika KKS4 kwa kuzingatia kanuni ya uwazi na uwekevu kama inavyosisitizwa na Kiango (2000) na Mdee (2010). Kwa upande wa KKF1, homonimu **nyanya¹** imefasiliwa tofauti na ilivyo katika KKS4 ikimaanisha ni *tunda jekundu likiwa limeiva* lakini KKF1 inasema ni *tunda kijani lenye umbo refurefu*. Hali hii husababisha fasili kuwa na utata. Ili kuondoa utata huo, KKF1 ingeweza kueleza kuwa **nyanya¹** ni *tunda la kijani likiwa halijaiva*. Pia, homonimu **nyanya²** imefasiliwa kwa kutumia urejeleano wa kisawe katika KKF1 wakati katika KKS4 imetoe fasili ya homonimu hiyo.

Aidha, makala haya yamebainisha kuwa kuna tofauti ya uingizaji wa maana za kihomonimu baina ya KKS4 na KKF1. Rejea data katika Mfano Na. 1 zinazothibitisha tofauti hii.

Mfano Na. 1: Tofauti za Uingizaji wa Maana za Kihomonimu katika KKS4 na KKF1
chochea **1** sogezasogeza au gusa kwa kijiti. **2** sababisha ugomvi vsw. chokoza, kasirisha, chipua. **3** tia hamu au shauku ya kufanya kazi. **4** chuma tunda kwa kutumia ncha ya jiti refu lisilokuwa na kigoe kwa kulisukuma kwa ncha ya jiti hili. (KKS4 uk. 79)

chochea¹ kitendo cha kusogeza vijinga vya moto jikoni ili moto uwake zaidi.

chochea² kitendo cha kuhamasisha watu wagombane.

chochea³ kitendo cha kupandisha utambi wa taa. (KKF1, uk. 52)

Data katika Mfano Na. 1 inaonesha kuwa kidahizo homonimu **chochea** kimeingizwa kama polisemi katika KKS4 wakati katika KKF1 kimeingizwa kama homonimu. Homonimu ni uhusiano wa maana kileksika ambapo umbo moja huwa na maana zaidi ya moja tofauti wakati polisemi ni hali ya neno moja kurejelea maana zaidi ya moja zenye uhusiano (Charwi, 2021). Tukirejelea mfano wa kwanza, maana za kidahizo **chochea** katika KKS4 zina uhusiano, ndiyo maana zimeingizwa kama polisemi. Kwa upande wa KKF1, maana 1 mpaka ya 3 zilizoingizwa kihomonimu zina uhusiano wa karibu kwani zote zinarejelea kitendo cha kufanya kitu kiongezeke. Hivyo, ni vyema zingeingizwa kama polisemi. Tofauti hii ya uingizaji wa vidahizo homonimu ni changamoto kwa mtumiaji wa kamusi kwani anawenza kuona kuwa ni homonimu kumbe ni polisemi hasa kwa wale wanaojifunza lugha, watafiti mbalimbali na watumiaji wa lugha husika. Kiango (2017) anasisitiza kuwa mtunzi wa kamusi anapaswa kuwa makini katika uingizaji wa vidahizo homonimu na polisemi kwani huweza kuchangamana. Hivyo, vidahizo homonimu viingizwe mara nyingi kutoptana na idadi ya maana zake kwa kuwa maana zake hazina uhusiano. Mwanaleksikografu anapaswa kutambua mipaka ya vidahizo polisemia na homonimu ili kuepusha huu mwingiliano ingawa ni vigumu kuweka mpaka maalumu kimaana baina ya homonimu na polisemi kama inavyodhihirishwa na Mwendamseke (2016). Jedwali Na. 5 linaonesha muhtasari wa tofauti za uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1.

Jedwali Na. 5: Muhtasari Unaooonesha Tofauti za Uingizaji wa Vidahizo Homonimu katika KKS4 na KKF1

KKS4	KKF1
1. Katika matamshi alfabeti chimeingizwa kama /tʃ/, ngimeingizwa kama /ŋ/.	1. Katika matamshi alfabeti chimeingizwa kama /č/ na /čʰ/, alfabeti ngimeingizwa kama /ng/.
2. Hakuna uchopekaji wa viyeyusho /w/ na /j/ panapokuwa na mfuatano wa irabu katika neno.	2. Kuna uchopekaji wa viyeyusho /w/ na /j/ panapokuwa na mfuatano wa irabu katika neno.
3. Mkazo umewekwa katika silabi ya pili kutoka katika mwisho wa neno.	3. Mkazo haujawekwa katika vidahizo vyote.
4. Hakuna sifa ya mpumuo katika matamshi.	4. Kuna sifa ya mpumuo katika matamshi ya baadhi ya vidahizo kwenye vipasuo vinavyounda silabi ya kwanza /kʰ/, /pʰ/ na /čʰ/.
5. Taarifa ya kietimolojia imeingizwa.	5. Hakuna taarifa ya kietimolojia katika vidahizo.
6. Taarifa ya uhusika wa vitenzi imeingizwa.	6. Hakuna taarifa ya uhusika wa vitenzi.
7. Maneno mengi katika KKS4 yana utoshelevu wa maana.	7. Baadhi ya maneno katika KKF1 yana maana finyu na za mzunguko.
8. Vidahizo vingi ambavyo ni homonimu vimeingizwa kwa kuzingatia utaratibu husika unaongoza uingizaji wa vidahizo vya aina hiyo.	8. Uwepo wa baadhi ya vidahizo kuingizwa kama homonimu badala ya kuingizwa kama polisemi.

5.2 Ufanano Unaajitokeza katika Uingizaji wa Kidahizo Homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Toleo la Nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Toleo la Kwanza

Pamoja na uwepo wa tofauti baina ya kamusi hizi mbili, matokeo ya makala haya yamebaini pia kuwa kuna ufanano katika uingizaji wa baadhi ya vidahizo homonimu. Ufanano huo umejidhihirisha katika uingizaji wa taarifa za kitahajia, kimatamshi, ubainishaji wa viambishi vya umoja na wingi na ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi.

5.2.1 Tahajia

Tahajia ni uwakilishi wa neno kwa kutumia herufi zinazowakilisha sauti zinazounda neno hilo (Kiango, 2017). Ni wazi kuwa tahajia huwakilisha sauti za lugha katika maandishi yanayounda neno. Katika kamusi, tahajia huzingatiwa ili kuwasilisha maneno kwa usahihi na kufuata kanuni na taratibu za lugha husika. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza, kuna ufanano wa uingizaji wa tahajia za baadhi ya homonimu. Rejea data katika Jedwali Na. 6 lifuatalo:

Jedwali Na 6: Ufanano wa Kitahajia katika Kuingiza Vidahizo Homonimu kwenye KKS4 na KKF1

KKS4		KKF1	
Tahajia	Uk.	Tahajia	Uk.
<i>anga</i> ¹ <i>anga</i> ²	19	<i>anga</i> ¹ <i>anga</i> ²	10
<i>doria</i> ¹ <i>doria</i> ²	104	<i>doria</i> ¹ <i>doria</i> ²	71
<i>fuko</i> ¹ <i>fuko</i> ² <i>fuko</i> ³	131	<i>fuko</i> ¹ <i>fuko</i> ² <i>fuko</i> ³	88
<i>gude</i> ¹ <i>gude</i> ²	154	<i>gude</i> ² <i>gude</i> ²	103
<i>kifimbo</i> ¹ <i>kifimbo</i> ²	249	<i>kifimbo</i> ¹ <i>kifimbo</i> ²	161
<i>mwezi</i> ¹ <i>mwezi</i> ²	465	<i>mwezi</i> ¹ <i>mwezi</i> ²	294
<i>ongoa</i> ¹ <i>ongoa</i> ²	506	<i>ongoa</i> ² <i>ongoa</i> ²	316
<i>rusu</i> ¹ <i>rusu</i> ²	554	<i>rusu</i> ¹ <i>rusu</i> ²	350
<i>wano</i> ¹ <i>wano</i> ²	726	<i>wano</i> ¹ <i>wano</i> ²	457

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Data katika Jedwali Na. 6 zinaonesha ufanano wa kitahajia katika uingizaji wa vidahizo homonimu kwenye KKS4 na KKF1. Vidahizo hivyo vimeingizwa kama homonimu katika kamusi zote mbili. Homonimu hizo zina ufanano wa kitahajia kwani kila homonimu othografia yake jinsi ilivyo katika KKS4 ndivyo ilivyo katika KKF1. Nadharia ya Metaleksikografija inasisitiza kuwa maandishi ya maneno yanayoingizwa kwenye kamusi yanapaswa kuwa sahihi ili kuepusha suitafahamu kwa mtumiaji wa kamusi. Kwa kutumia mhimili wa kuhakiki kamusi, matokeo yamedhihirisha ufanano huo katika vidahizo homonimu katika kamusi hizi mbili. Tahajia sanifu ya kidahizo ndiyo hutafutwa na mtumiaji wa kamusi sanifu. Hivyo, kuna umuhimu wa kuingiza tahajia za vidahizo kwa usanifu na ufasaha ili kukidhi hitaji la watumiaji wa kamusi hizo.

5.2.2 Matamshi

Makala haya yamebaini kuwa kuna ufanano wa matamshi kwa baadhi ya vidahizo homonimu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la nne na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* toleo la kwanza. Imebainika kuwa ufanano wa matamshi uliopo ni ule wa sauti zinazohusika katika kidahizo kama Jedwali Na. 7 linavyodhihirisha.

Jedwali Na. 7: Ufanano wa Kimatamshi (hasa wa sauti) katika Uingizaji wa Vidahizo Homonimu kwenye KKS4 na KKF1

KKS4			KKF1		
Kidahizo	Matamshi	Uk.	Kidahizo	Matamshi	Uk.
ala¹	/'ala/	11	ala¹	/ala/	06
ala²	/'ala/		ala²	/'ala/	
baa¹	/'ba:/	28	baa¹	/ba:/	14
baa²	/'ba:/		baa²	/'ba:/	
baa³	/'ba:/		baa³	/'ba:/	
data¹	/'data/	92	data¹	/data/	63
data²	/'data/		data²	/'data/	
lifti¹	/'lifti/	328	lifti¹	/lifti/	210
lifti²	/'lifti/		lifti²	/'lifti/	
ndege¹	/'ndEgE/	477	ndege¹	/ndEgE/	301
ndege²	/'ndEgE/		ndege²	/'ndEgE/	
peta¹	/'peta/	525	peta¹	/peta/	330
peta²	/'peta/		peta²	/'peta/	
rafu¹	/'rafu/	542	rafu¹	/rafu/	342
rafu²	/'rafu/		rafu²	/'rafu/	
tupa¹	/'tupa/	650	tupa¹	/tupa/	406
tupa²	/'tupa/		tupa²	/'tupa/	

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Data katika Jedwali Na. 7 zinaonesha kuwa kuna ufanano wa uingizaji wa matamshi (hasa katika sauti) wa vidahizo homonimu katika kamusi zote mbili KKS4 na KKF1 licha ya kuwa KKS4 imezingatia kuweka mkazo katika matamshi ya vidahizo. Matamshi hayo yamebainishwa kwa alama za mwaju //. Nadharia ya Metaleksikografia inaeleza kuwa uhakiki wa vipengele vinavyoingizwa kwenye kamusi kama sauti za vidahizo ni muhimu kufanyika kwa umakini ili kuwasaidia watumiaji wa kamusi kupata matamshi sahihi ya lugha husika kama inavyotumiwa na wazawa. Hivyo, taarifa ya matamshi katika kamusi ni muhimu sana.

5.2.3 Ubainishaji wa Viambishi vya Umoja na Wingi

Dhana ya umoja na wingi inayowasilishwa katika kipengele hiki ni maumbo ya nomino ambayo yanaweza kuchukua viambishi vya wingi na au umoja. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa maumbo yaliyoingizwa kama vidahizo homonimu katika kamusi za KKS4 na KKF1 ni maumbo ya umoja kwa zile nomino zenye umoja na wingi. Kwa nomino zenye umbo moja, zimeingizwa kama zinavyotumika, kwa mfano, **nywele, masazo na maziwa**. Rejea data katika Jedwali Na. 8.

Jedwali Na. 8: Ufanano wa Uingizaji wa Maumbo ya Umoja na au Wingi kwa Vidahizo Homonimu katika KKS4 na KKF1

Kidahizo homonimu	Umoja na Wingi katika KKS4	Uk.	Umoja na Wingi katika KKF1	Uk.
behewa¹ behewa²	(ma-) (ma-)	42	(ma-) (ma-)	24
choo¹ choo² choo³	(vy-) (-) (-)	81	(vy-) (vy-) (-)	55
fuko¹ fuko²	(ma-) (ma-)	131	(ma-) (ma-)	88
kanga¹ kanga²	(-) (-)	221	(-) (-)	143
mdudu¹ mdudu²	(wa-) (-)	379	(wa-) (-)	239
sera¹ sera²	(-) (-)	569	(-) (-)	359
tambo¹ tambo² tambo³	(-) (ma-) (ma-)	615	(-) (ma-) (ma-)	386

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Data katika Jedwali Na. 8 zimeingizwa kama vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. **Vidahizo behewa, fuko na tambo** vimeingizwa kama homonimu ambazo zina umbo la wingi (ma-) ambalo limeingizwa sawa katika kamusi zote mbili. Pia, homonimu **choo¹** inawasilishwa ikiwa na umbo la wingi (vy-) wakati homonimu **choo³** ikiwekewa umbo la kapa (-) katika kamusi zote mbili. Vidahizo **kanga** na **sera** ni vidahizo homonimu visivyo na umbo la wingi katika KKS4 na KKF1. Halikadhalika, homonimu **mdudu¹** ina umbo la wingi (**wa-**) wakati mdudu² ina umbo la umoja tu katika kamusi zote mbili. Hivyo, data hii inadhihirisha kuwa kuna ufanano wa uingizaji wa maumbo ya umoja na wingi kwa baadhi ya vidahizo homonimu katika kamusi teule.

Katika kamusi ya KKS4 na KKF1, viambishi vya umoja na wingi vimeoneshwa vikiwa katika mabano ya mduara (). Viambishi vya umoja na wingi katika vidahizo nomino vinawakilisha ngeli za nomino. Kwa kuzingatia msingi wa uhakiki wa kamusi katika Nadharia ya Metaleksikografie, makala yamebaini kuwapo kwa ufanano wa urejeleaji wa viambishi vya umoja na wingi katika KKS4 na KKF1. Hivyo, matokeo haya yanadhihirisha kuwa kamusi zote mbili zimeonesha uzingativu wa kipengele hiki muhimu cha taarifa za kisarufi zinazopaswa kuingizwa katika kamusi. Kipengele hiki ni muhimu sana kwa kamusi zinazolenga kuhifadhi na kuendeleza usanifu na ufasaha wa lugha husika kwa watumiaji wake.

5.2.4 Ubainishaji wa Viambishi vya Upatanisho wa Kisarufi

Upatanisho wa kisarufi ni hali ya viambishi vya maneno ndani ya tungo kukubaliana na kushikamana ili kuleta maana iliyokusudiwa (Ndumba, 2021). Katika kipengele hiki, data zimechambuliwa kwa kuangalia ufanano wa vidahizo homonimu katika ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi kwenye KKS4 na KKF1. Rejea data katika jedwali na. 9.

Jedwali Na. 9: Ufanano wa Upatanisho wa Kisarufi katika Uingizaji wa Vidahizo Homonimu kwenye Kamusi za KKS4 na KKF1

Kidahizo Homonimu	Upatanisho wa Kisarufi katika KKS4	Uk.	Upatanisho wa Kisarufi katika KKS4	Uk.
baka ¹ baka ²	li-/ya- -	32	li/ya -	16
karara ¹ karara ²	li-/ya- li-/ya-	225	li/ya li/ya	145-146
mkunga ¹ mkunga ²	a-/wa- a-/wa-	406	a/wa a/wa	256
shina ¹ shina ²	li-/ya- li-/ya-	579	li/ya li/ya	364
tanzu ¹ tanzu ²	i-/zi- -	619	i/zi -	388
ubani ¹ ubani ²	u- u-	657	u u	411

Chanzo: TUKI (2019) na BAKIZA (2010)

Vidahizo katika Jedwali Na. 9 vimeingizwa kama homonimu katika KKS4 na KKF1. Viambishi (li-, ya-), (a-/wa-), (i-/zi-) na (u-) vimeingizwa katika vidahizo homonimu vya kamusi zote mbili kuwakilisha upatanisho wa kisarufi katika matumizi. Taarifa ya upatanisho wa kisarufi katika kamusi zinazolenga kuzingatia usanifu wa lugha ni muhimu sana kama Nadharia ya Metaleksikografia ya Wiegand (1984) inavyositisiza kuwa uingizaji wa upatanisho wa kisarufi katika kamusi ni kipengele kinachomsaidia mtumiaji wa kamusi kuelewa semantiki pamoja na kupata ujuzi wa kisintaksia pale anapohitaji kutumia kidahizo husika kuunda sentensi.

Hivyo, katika lengo hili matokeo yanaonesha kuwa hata kama zipo tofauti za uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1, bado kuna ufanano katika uingizaji wa baadhi ya taarifa katika kamusi hizi. Ufanano huo umejidhihirisha katika vipengele vya tahajia, matamshi, ubainishaji wa viambishi vya umoja na wingi pamoja na ubainishaji wa viambishi vya upatanisho wa kisarufi.

6.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yamechunguza tofauti na ufanano wa uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1. Matokeo yanaonesha kuwa kuna tofauti katika uingizaji wa vidahizo hivyo baina ya kamusi hizi mbili kwa udhihirisho wa namna matamshi yalivyoingizwa kupitia taarifa za kietimolojia, uhusika wa vitenzi pamoja na uingizaji wa fasili za maana. Baadhi ya tofauti zinasababishwa na tofauti za kitamaduni na maeneo ya kijiografia baina ya watumiaji wa kamusi hizi mbili ambamo lugha ya Kiswahili inatumika. Kwa ujumla, taarifa zilizoingizwa katika KKS4 ni nyingi kuliko taarifa zilizoingizwa katika KKF1. Hata hivyo, makala haya yamedhihirisha kuwapo kwa ufanano wa uingizaji wa vidahizo homonimu katika KKS4 na KKF1 katika vipengele vyta tahajia, matamshi, ubainishaji wa viambishi vyta umoja na wingi pamoja na ubainishaji wa viambishi vyta upatanisho wa kisarufi. Kutokana na matokeo ya makala haya, inapendekezwa kuwa ni vema kuwe na kanuni na taratibu ambazo zitakuwa ndiyo mwongozo wa kuzingatia katika utunzi wa kamusi kwa taasisi husika na kwa watu binafsi. Jambo hili litaondoa mkanganyiko wanaoupata watumiaji wa kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili nchini Tanzania, Afrika Mashariki na hata nchi nyingine ambako Kiswahili kinatumika. Kwa upande wa watunzi wa KKS4 na KKF1, ni vyema wakushughulikia katika matoleo yanayofuata yale yaliyoonekana kuwa ni tofauti zenyetupungufu ili kuwa na kamusi zenyetutongelevu zaidi. Aidha, makala haya yanaona kuwa kuna umuhimu wa kuwapo kwa umoja na ushirikiano baina ya mabaraza au taasisi zinazohusika na utungaji wa kamusi ili kupunguza tofauti zinazojitokeza katika utunzi huo. Hata hivyo, kwa kuwa makala haya yamejikita katika kulinganisha vidahizo homonimu, kipengele cha polisemi kinaweza pia kikafanyiwa uchunguzi.

Marejeleo

- Andrew, J. S. (2016) *Uingizaji wa Homonimu, Polisemi na Sinonimu katika Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010). Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- BAKIZA (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Kenya: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Charwi, M. Z. (2021) "Chanzo cha Tofauti za Kileksika na Maana Zake Tanzania Bara na Visiwani na Athari Zake kwa Watumiaji wa Kiswahili." *Mulika*, Juz. Na. 40(2): 42-59.
- Gichuru, T. M. (2020) *Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kale na Kisasa*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Haji, M. N. (2018) *Muundo wa Kirai Kitenzsi katika Lahaja ya Kitumbatu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Hans, M. M. (2017) “*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004): Changamoto na Namna ya Kukabiliana Nazo.” *Kiswahili*, Juz. Na. 75(1): 52-63.
- Kiango, J. G. (2000) *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Entries*. Tokyo, Japan: Institute for the Study of Language and Cultures of Asia and Africa.
- Kiango, J. G. (2017) “Usawidi wa Vitomeo vya Kamusi.” *Mulika*, Juz. Na. 23: 75-94.
- Maithulia, M. I. (2021) *Urejeleano katika Utunzi wa Kamusi za Kiswahili: Uchanganuzi Linganishi wa Kamusi Teule za Lugha Moja*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Matinde, R. S. (2012) *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia, kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Education Publishers Ltd.
- Mbaabu, I. (2007) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J. S. (2010) *Nadharia na Historia ya Leksikografija*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2011) *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mdee, J. S. (2012) *Dictionaries and the Standardization of Spelling in Swahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mwendamseke, F. (2016) “Uelekeo wa Maana za Kipolisemia katika Msamiati wa Kiswahili: Mifano kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu.” *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 14: 39-49.
- Ndumba, K. N. (2021) *Uchanganuzi wa Kimofosintaksia wa Viangami katika Lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Okal, O. B. (2018) “Uhakiki Linganishi wa Taarifa Muhimu kuhusu Vidahizo katika *Kamusi ya Karne ya 21* na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.” *Mulika*, Juz. Na. 36: 87-100.
- TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: Oxford University Press, East Africa Limited.
- Weigand, E. H. (1984) “On the Structure and Contents of a General Theory of Lexicography.” Katika R. Hartmann (Mh.), *LEXeter '83: Proceedings: Papers from the International Conference on Lexicography at Exeter, 9–12 September 1983*. Berlin, Boston: Max Niemeyer Verlag. kur. 13-30.